



JE, CHANJO NI NINI?

**Imetengenezwa na
Asian Media Access
na Spitfire**

Kila mmoja wetu amefanya mabadiliko katika maisha yake kwa sababu ya COVID-19. Shughuli zetu za kila siku zimebadilika, kama vile kufanyia kazi au kusomea nyumbani, kuvaa barakoa, au kukaa futi sita mbali na marafiki na jamaa zetu.

Mojawapo ya nyenzo za kudumisha usalama wa jumuiya zetu dhidi ya COVID-19 ni chanjo. Chanjo ni kama mkanda wa usalama kwa mfumo wetu wa kinga. Mfumo wa kinga ni mfumo wa ulinzi wa mwili unaopigana na ugonjwa na kutuweka tukiwa wenye afya. Kama vile tunavyofunga mikanda ya usalama ili kubaki salama iwapo ajali itatokea, vivyo hivyo kupata chanjo hutusaidia kubaki wenye afya wakati virusi kama COVID-19 vinaenea.

Chanjo hufanya kazi kwa kufunza mfumo wa kinga ya mwili wetu kupigana na ugonjwa. Ikiwa tutapatwa na virusi hivyo, miili yetu itaweza kuitikia haraka. Hiyo hutulinda tusiwe wagonjwa sana au kuhitaji kwenda hospitalini.

Mwili wetu unapojua jinsi ya kupigana na kirusi, hiyo inaitwa kinga. Chanjo huwapa watu wengi kinga, ambapo inamaanisha kwamba virusi hivyo haviwezi kuenea kwa umma kwa urahisi. Virusi vinapoenea, vinaweza kubadilika kuwa aina mpya. Chanjo husaidia kukomesha virusi visibadilike na kuwa aina mpya inayosababisha madhara zaidi.



Chanjo zimesaidia jumuiya nyingi kupigana na virusi kwa zaidi ya miaka 100. Chanjo ilipigana na ndui, surua na polio na ndiyo sababu kuu ya hivi virusi hatari kukosa kuwepo kwa wingi leo. Kutokana na ujuzi wa kukabiliana na ndui na virusi vingine, wanasayansi walitengeneza chanjo salama na zenye ufanisi za kukabiliana na COVID-19. Teknolojia na viambato vilivyotumiwa kwa chanjo za COVID-19 vilifanyiwa utafiti kwa makumi ya miaka.

Kampuni tatu (Pfizer, Moderna, na Johnson & Johnson) walitengeneza chanjo za COVID-19 zilizo salama na zenye ufanisi. Viambato vya chanjo ni sawa na viambato vya chakula. Vimetengenezwa na mRNA, mafuta, sukari na chumvi. Kama vile chakula, viambato vya chanjo huondoka kwenye mwili wako baada ya kufanya kazi yake. mRNA ndicho kiambato kinachosababisha chanjo za Pfizer na Moderna kufanya kazi. mRNA ni molekuli inayoupa mfumo wa kinga maelekezo ya jinsi ya kupigana na virusi. Molekuli hizo zisizo na madhara huwezesha mfumo wetu wa ulinzi kufanya mazoezi ya kupigana na COVID-19 na kujenga ulinzi imara.

	Pfizer-BioNTech	Moderna	Johnson & Johnson
Kiambato amilifu:	mRNA	mRNA	Vekta (kipande cha kirusi kilichofifishwa kinachosaidia mfumo wa kinga kujenga ulinzi)
Kwa umri wa miaka:	5+	18+	18+
Dozi:	2 + kiongeza nguvu	2 + kiongeza nguvu	1 + kiongeza nguvu
Ufanisi:	95%	95%	67%

Kila chanjo ilipitia vipindi vitatu vikali vya utafiti na majaribio ili kuhakikisha kwamba zote ni salama na zenye ufanisi. Kila chanjo pia ilipata idhini mbili. Moja ilitoka Food and Drug Administration (FDA), ambalo ni shirika la serikali linalowajibika kuhakikisha usalama wa dawa. Nyingine ilikuwa kutoka kwa Kamati ya Ushauri Kuhusu Mazoea ya Chanjo (Advisory Committee on Immunization Practices). Hawa ni wataalamu wa matibabu na afya wanaotengeneza miongozo ya kutumia chanjo kwa usalama.



Tangu chanjo hizo ziidhinishwe mwezi Desemba 2020, zaidi ya watu milioni 255 nchini Marekani wamezitemia. Hiyo ndiyo sababu ni salama zaidi sasa kurudi shule na kazini. Pia ni salama zaidi kuwaona wapendwa wetu ana kwa ana. Kuchanjwa ni bila malipo na ni rahisi. Kliniki za mitaa, maduka ya dawa, na vituo vya afya katika jumuiya yako zinatoa chanjo bila malipo. Huhitaji bima ya afya au kitambulisho ndipo upate chanjo.

Baada ya kupata chanjo, ni kawaida kujihisi mgonjwa kidogo. Unaweza kuvimba mkono, kuumwa na kichwa, uchovu, maumivu ya misuli, baridi, joto au kichefuchefu. Hizi ni dalili kwamba chanjo inafanya kazi. Mwili wako unajifunza kupigana na virusi hivi.

COVID-19 ni hatari hasa kwa watu wazima na watu wenye matatizo mengine ya kiafya. Miili yao haiwezi kupigana na virusi kwa njia nzuri. Chanjo zinaweza kusaidia kuwalinda watu hawa dhidi ya virusi hivi. Ikiwa kuna mzee au mtu aliye na matatizo ya afya katika familia yako, kuchanjwa kunalinda afya yao na yako.

COVID-19 imesababisha miaka miwili iliyopita kuwa ya kutisha na yenye balaa. Lakini unaweza kudhibiti afya yako na kulinda jumuiya yako kwa kupata maelezo zaidi kuhusu chanjo. Madaktari na wauguzi wako tayari kujibu maswali yako na kupunguza wasiwasi wako. Kwa hivyo, endelea kuuliza maswali na kuzungumza na familia yako na marafiki kuhusu walivyohisi baada ya kuchanjwa. Hiyo itakusaidia kuamua kama chanjo ni sawa kwako na jumuiya yako.

**ROLL UP YOUR SLEEVES,
VACCINE ADVOCATES!**

STAY SAFE MN

- ✓ Get your shot
- ✓ Share on social media
- ✓ Encourage at least 3 other people to get vaccinated